

7. Huduma zinazohusiana na afya

Kuna wataalamu wengi wa afya ambao wamefunzwa kutibu shida mahsusi za kiafya ambao wanaitwa 'wataalamu wanaohusiana na huduma za afya' (allied health). Wataalamu hawa wanaweza kufanyakazi katika hospitali, vituo vya matibabu, kliniki na misala ya kibinafsi. Baadhi ya huduma hizi zina usaidizi kutoka kwa Medicare. Ni vyema ikiwa utahakikisha kama kuna usaidizi wowote kutoka Medicare kabla ya kufanya miadi ya kuonana na wataalamu hawa. Kampuni nyingi za bima ya afya hutoa usaidizi kwa huduma kama hizi..

	<p>Upimaji Masikio</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ wataalamu wa kupima usikiaji ni wataalamu maalum katika makadirio (Mapimo), kuzuia na kutoa mauguzi yasiotumia dawa katika taathiri ya masikio na madhara yanayo husiana na mafahamiano. ■ Wataalamu hawa wanakadiri (Kupima) usikiaji katika watoto wachanga, watoto na watu wazima, na wanahusika katika mipango ya marekebisho ■ wataalamu wa kupima kusikia hufanyakazi hospitalini, huduma za jamii na misala ya kibinafsi. Ikiwa una hoja yoyote kuhusu kusikia kwako au kusikia kwa mtoto wako, muulize daktari wako wa familia kuhusu kupata rufaa ya kwenda kuonana na wataalamu hawa. ■ Shirika la Upimaji kusikia la Australia www.audiology.asn.au
	<p>Lishe na Mwiko</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Wataalamu wa lishe huwasaidia watu kuelewa uhusiano kati ya chakula na afya ili waweze kufanya uchaguzi bora wa ulaji wenye manufaa. ■ Wataalamu hawa wanaweza kufanya kazi katika hospitali za umma, vituo vya afya vya jamii na pia kibinafsi. ■ Medicare husimamia katika baadhi ya huduma hizi chini ya Mpango wa Msingi wa Kuboresha maangalizi. Muulize daktari wako wa familia (GP) kuhusu huduma hizi. ■ Shirika la Wataalamu wa lishe la Australia www.daa.asn.au
	<p>Tiba ya kazini</p> <ul style="list-style-type: none"> ■ Mtaalamu wa tiba ya kazini husaidia watu kushirikiana katika maisha ya kila siku. Wafanyi kazi wanaweza kuwa na upungufu wa uwezo wa kufanya kazi fulani kwa sababu ya ugonjwa, ulemavu au jeraha ■ Mtaalamu wa tiba ya kazini anaweza kufunza mbinu mpya ya kufanya kazi, kutoa vifaa ambavyo vinampa mtu uhuru wa kufanya kazi, kupunguza viziwi katika mazingira ya kazini na kuwasaidia watu kuzoea mazingira hayo. ■ Medicare husimamia katika baadhi ya huduma hizi chini ya Mpango wa Msingi wa Kuboresha maangalizi. Muulize daktari wako wa familia (GP) kuhusu huduma hizi. ■ Wataalamu hawa wanafanya kazi katika hospitali, vituo vya afya vya jamii na pia kibinafsi ■ Shirika la Australia la Wataalamu wa Tiba ya Kazini www.ausot.com.au

Karatasi hii ya kweli iko katika mfululizo wa 10. idadi kamili:

1. Mfumo wa afya nchini Queensland
2. Kumwona daktari
3. Madawa
4. Hospitali za Queensland
5. Vituo vya afya ya jamii
6. Huduma za meno
7. Afya ya pamoja
8. Kuishi na afya na kuzuia magonjwa
9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu
10. Wewe na mfumo wa huduma ya afya